

Anwani ya simu: "REGCOM COAST"  
Simu Na. 02-2402500.  
Fax Na. 02-2402250/2402686/2402151  
Barua pepe: [ras@pwani.go.tz](mailto:ras@pwani.go.tz)  
[ras.pwani@proraly.go.tz](mailto:ras.pwani@proraly.go.tz)



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
Mkoa wa Pwani,  
S. L. P 30080,  
**KIBAHA.**

## **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

### **TAMKO LA MKUU WA MKOA WA PWANI KUZUIA UFUNGASHAJI, UUZAJI NA UNUNUZI WA BIDHAA KWA MTINDO WA LUMBESA**

SHERIA YA VIPIMO MAPITIO YA MWAKA 2002 SURA 340 KIFUNGU 54 (1) (c) (p) NA KANUNI ZAKE ZA MWAKA 2008 KAMA ZILIVYOTANGAZWA KWENYE GAZETI LA SERIKALI GN. 16 INAKATAZA KUFUNGASHA, KUUZA NA KUNUNUA BIDHAA KWA KUTUMIA VIPIMO VISIVYO RASMI. VIPIMO HIVYO KWA MAJINA YALIYOZOELEKA KWENYE MAZAO YA KILIMO NA MISITU VINAITWA LUMBESA NA AU KANGOMBA (KWA ZAO LA KOROSHO).


JEDWALI NAMBA 11, KIFUNGU 26 (1)(b) LA SHERIA HIYO LIMETOA ORODHA YA BIDHAA NA VIPIMO VINAVYOTAKIWA KUTUMIKA WAKATI WA UFUNGASHAJI. HAPA NITATAJA BAADHI YA BIDHAA ZINAZOZALISHWA ZAIDI MKOANI PWANI NA VIPIMO VINAVYOTAKIWA KUTUMIKA, KAMA IFUATAVYO:

- |    |                              |                     |
|----|------------------------------|---------------------|
| 1. | MAHINDI/ MTAMA               | - GUNIA LA KILO 90  |
| 2. | MKAA                         | - GUNIA LA KILO 30  |
| 3. | KUNDE/CHOROKO/MBAAZI/KARANGA | - GUNIA LA KILO 90  |
| 4. | MPUNGA                       | - GUNIA LA KILO 75  |
| 5. | MICHELE                      | - GUNIA LA KILO 100 |
| 6. | UFUTA                        | - GUNIA LA KILO 90  |
| 7. | ALIZETI                      | - GUNIA LA KILO 40  |
| 8. | KOROSHO                      | - GUNIA LA KILO 80  |

PAMOJA NA HITAJI LA KUTEKELEZA SHERIA ILIYOTAJWA NA KANUNI ZAKE, LUMBESA PIA INA MADHARA MAKUBWA NA ZAIDI INAATHIRI UCHUMI WA MKOA NA TAIFA KAMA IFUATAVYO:

1. LUMBESA INASABABISHA SERIKALI KUKUSANYA MAPATO PUNGUFU
2. LUMBESA INAATHIRI MIUNDOMBINU, HASA BARABARA, MADARAJA NA MABOMBA
3. LUMBESA INAMPUNJA MKULIMA/ MZALISHAJI
4. LUMBESA INAATHIRI AFYA ZA WABEBAJI HIVYO KUPUNGUZA NGUVU KAZI YA TAIFA
5. LUMBESA INAATHIRI MAISHA, MALI NA KUONGEZA WATEGEMEZI KUTOKANA NA AJALI, MAGONJWA NA VIFO

KUTOKANA NA HITAJI LA KUTEKELEZA SHERIA TAJWA NA KANUNI ZAKE NA ILI KUONDOA ATHARI ZINAZOTOKANA NA LUMBESA, NINATOA TAMKO KWAMBA, "NI MARUFUKU KWA WAKULIMA, WAZALISHAJI NA WAFANYABIASHARA MKOANI PWANI KUFUNGASHA, KUUZA AU KUNUNUA BIDHAA KWA MTINDO WA LUMBESA AU KANGOMBA (KWA ZAO LA KOROSHO) KUENZIA LEO TAREHE 25 APRILI, 2016. WALE WOTE WATAKAOKAIDI TAMKO HILI WATAADHIBIWA KWA MUJIBU WA SHERIA ILIYOTAJWA. TAASISI ZOTE ZA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SHERIA ZISIMAMIE TAMKO HILI NA KUCHUKUA HATUA STAHIKI KWA WALE WOTE WATAKAOKIUKA".



ENG. EVARIST WELLE NDIKILO

**MKUU WA MKOA**

**PWANI**